

CHANJO YA COVID-19 YA JOHNSON & JOHNSON (JANSSEN)

061421 SWAHILI

Chanjo ya Johnson & Johnson/Janssen (J&J) ni mojawapo ya chanjo tatu za COVID-19 zinazopatikana kwa ajili ya watu wazima nchini Marekani. Ni kawaida kuwa na chanjo zaidi ya moja ili kupambana na virusi vya aina moja.

Chanjo zote zinazopatikana ni nzuri katika kulinda dhidi ya homa kali, kulazwa na kifo kinachosababishwa na COVID-19. Zote zinapendekezwa na wataalamu wa afya.

Mwili wako utakuwa umeshajiandaa kukukinga wiki 2 baada ya dozi moja tu ya chanjo ya J&J.



Inachofanya

Chanjo ya J&J ni chanjo spesheli ya virusi. Ina virusi vya adeno visivyo na madhara (virusi vya kawaida vya mafua), ambavyo vinabeba jeni kutoka kwenye protini ya mwiba ya virusi vya korona. Hii inaufundisha mwili wako kutambua na kupambana na virusi vya korona vinavyosababisha COVID-19, kama chanjo nyingine zilizoidhinishwa (Pfizer na Moderna).

Isichofanya

- Haikuambukizi COVID-19 au mafua.
- Haibadilishi DNA yako au vinasaba vyako.
- Haisababishi utasa.

Je, Chanjo ya COVID-19 ya Johnson & Johnson imetengenezwakwa kutumia nini?

Chanjo ya J&J ina virusi vya adeno vilivyoboreshwa kwa kutumia taarifa za virusi vya korona. Pia ina viungo vinavyosaidia kuifanya kuwa imara: chumvi, sukari na michanganyo mingine ya kaboni.

Chanjo hii haina mayai, vihifadhi, lateksi, nyama ya nguruwe au bidhaa nyingine za wanyama, au chembe hai za virusi vya korona.

Chanjo ya J&J ni kwa ajili ya watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi

Zungumza na daktari au kliniki yako iwapo una ujauzito au unanyonyesha, una mizio mkali, una historia ya kuganda damu au unatumia vipunguzi vya damu.

Madhara ya Chanjo

Watu wengi wanapata madhara madogo baada ya kupata chanjo. Hii ni ishara kwamba mwili wako unafanya kile kinachopaswa kufanya: kujenga kinga dhidi ya ugonjwa. Hata kama hujapata madhara ya chanjo, chanjo inafanya kazi kukulinda.

- Madhara yanayotokea sana ni pamoja na maumivu au wekundu mahali ulipodungwa sindano ya chanjo, maumivu ya kichwa, uchovu, na/au homa ndogo.
- Dalili hizi mara nyingi huondoka zenyewe baada ya siku chache. Zisipoondoka, mpigie simu daktari au kliniki yako.



Matatizo adimu, lakini makubwa

Athari ya mzio

Ni adimu, lakini baadhi ya watu huwa na athari mbaya ya mzio inayosababishwa na chanjo ya COVID-19. Kila mmoja anaombwa kusubiri kwa muda kidogo baada ya kupatiwa chanjo ili kuhakikisha kuwa hakuna athari mbaya ya mzio. Muda huu wa kusubiri unatoa wasaa wa matibabu ikihitajika.

Tatizo la damu kuganda

Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Serikali ya Jimbo wameshauri kuendelea kutumia chanjo ya Johnson & Johnson (J&J) baada ya siku 10 za kusitishwa mwezi Aprili, 2021. Usitishaji ulifanywa ili kuwasaidia wataalamu wa tiba kufahamu vizuri zaidi hatari ya aina adimu ya kuganda damu iliyoripotiwa baada ya watu wachache kupatiwa chanjo hii.

Tatizo hili baya ni kuganda kwa damu kunakohusisha mishipa ya damu katika ubongo, tumbo au miguu pamoja na viwango vya chini vya chembe sahani (aina ya chembehai za damu ambazo huusaidia mwili wako kuzuia kutokwa damu). Inaitwa mvilio wa damu pamoja na tatizo la kuwa na kiwango kidogo cha chembe sahani, au TTS. Tatizo hili ni baya sana na linaweza kusababisha kifo, lakini pia linaweza kutibika na kupona kabisa. Matibabu ni tofauti na yale ya ugandaji damu mwingine.

TTS ni nadra sana. Wataalam wanakadiria karibu wanawake 7 ya milioni 1 waliopata chanjo wenye umri wa miaka 18 na 49 wanaweza kukabiliwa na hili. Kwa wanawake wenye umri wa miaka 50 na zaidi na wanaume wa rika zote, tatizo hili baya ni nadra zaidi, ingawa limetokea.

Wataalamu wa tiba ambao walichunguza TTS kwa wagonjwa ambao wamepokea chanjo ya Johnson & Johnson waliamua kwamba kwa watu wengi faida za kupatiwa chanjo ya Johnson & Johnson zinazishinda hatari zake. Hatari ya kuganda damu au kufa kwa sababu ya ugonjwa wa COVID-19 ni kubwa sana kuliko hatari ya kuganda damu na kufa kwa sababu ya chanjo.

Chukua tahadhari zaidi dhidi ya dalili hizi hatari sana kwa wiki tatu baada ya kupata chanjo hii:

- maumivu makali ya kichwa au maumivu ya kichwa yasiyoisha
- kutoweza kuona vizuri
- maumivu ya kifua au maumivu makali ya tumbo
- kuvimba au maumivu ya miguu
- kupumua kwa shida
- kuchubuka kwa urahisi au madoa madogo ya damu kwenye ngozi yako nje ya sehemu uliyodungwa sindano

Iwapo utapata dalili zozote kati ya hizi, piga simu 911 au nenda kwenye chumba cha dharura. Ni muhimu kuwafahamisha kwamba ulipatiwa chanjo ya Johnson & Johnson hivyo watakuhudumia kwa njia ifaayo.

Kubaki salama

COVID-19 bado inaenea katika jamii zetu na hakuna chanjo iliyo na ufanisi wa 100%. Hata baada ya kupata chanjo, endelea kunawa mikono yako, vaa barakoa kwenye maeneo ya umma, dumisha umbali kati yako na watu wengine na punguza ukubwa na urefu wa mikusanyiko ama kukutana tu na watu wengine waliopata chanjo.

Tafuta “COVID-19” kwenye tovuti ya county yako ili kupata taarifa ya mahali husika.

